



ILANI KUHUSU UKUSANYAJI NA UTUMIAJI WA DATA BINAFSI

Maagizo kwa wafanyakazi: Waraka huu unaeleza kuhusu maelezo ambayo Shirika la Msalaba Mwekundu la Marekani hukusanya kutoka kwa watu wanaotafuta msaada wa kupata jamaa aliyepotea na jinsi tunavyotumia maelezo hayo. Tafadhali soma yaliyomo kwenye waraka huu kwa anayeuliza.

Shirika la Msalaba Mwekundu la Marekani linashirikiana na wanachama wengine wa Shirika la Msalaba Mwekundu la Kimataifa na Vuguvugu la Red Crescent ili kusaidia kubainisha hatima na mahali walipo watu waliopotea na kurejesha na kudumisha muunganisho kati ya familia zilizotengwa kutokana na mgogoro wa kivita, uhamiaji na janga asilia.

Ili kukusaidia kupata jamaa yako, Shirika la Msalaba Mwekundu la Marekani linahitaji kukusanya na kutumia maelezo kukuhusu na jamaa wako unayemtafuta. Ninaenda kueleza jinsi tunavyotumia na kushiriki maelezo na kukuuliza maswali fulani ili kupata idhini yako. Taarifa hii inapatikana kwenye tovuti yetu katika www.redcross.org/familylinks.

Tutahitaji kushiriki maelezo yako, ikijumuisha data yako ya kibinafsi na data ya kibinafsi ya jamaa yako unayemtafuta, na mashirika mengine ambayo yanaweza kusaidia katika kutafuta jamaa yako. Haswa, tunaweza kuhitaji kushiriki data na:

- Wanachama wengine wa Shirika la Msalaba Mwekundu/Vuguvugu la Red Crescent, haswa ICRC na jamii ya Msalaba Mwekundu/Red Crescent katika nchi au makazi yako na jamii ya kitaifa katika nchi au makazi ya jamaa yako
- Mashirika Mengine ya Kimataifa, kama vile Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) na mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN);
- Mashirika mengine ya ndani ya nchi, kama vile mashirika yanayotoa huduma za kijamii kwa jamii za ndani ya nchi;
- Mamlaka za serikali; na
- Makundi yasiyo ya serikali yaliyojiami.

Pia inawezekana kwamba sisi (au shirika linalosaidia katika utafutaji) litahitaji kufichua maelezo kwa wengine wakati wa shughuli ya utafutaji na/au kuchapisha baadhi ya maelezo, kama vile mabango, tovuti au matangazo ya umma kuhusiana na watu waliopotea.

Tutatumia maelezo ambayo umetupa kwa shughuli tu za kusaidia kubainisha hatima na mahali walipo watu waliopotea. Tutafuata masharti yoyote ya kisheria kushiriki data.

Tafadhali wasiliana na Shirika la Msalaba Mwekundu la Marekani kupitia [phone number, office address, email address] ikiwa una swali au wasiwasi kuhusu kesi yako au data yako ya kibinafsi.